# TANGAZO

## MKOPO WA HAZINA KWA WATUMISHI WA UMMA
## FUNGU 82N2

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Tunduru anawatangazia watumishi wa Halmashauri ya Wilaya kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru imepokea fedha kwa ajili ya kutoa mikopo kwa watumishi wa Umma kutoka Wizara ya Fedha na Mipango (Hazina).

Kwa mantiki hiyo, mnaelekezwa kuwa watumishi wote wenye sifa waandike barua za kuomba mikopo hii kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo;-

i. Mwombaji awe ni mtumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru anayekopesheka,
ii. Mfumo huu wa mikopo haununui madeni kutoka taasisi nyingine za mikopo,
iii. Mwombaji asiwe mwenye rekodi mbaya ya matukio ya kinidhamu au jinai,
iv. Mwombaji lazima awe amethibitishwa kazini ili aweze kuomba mkopo,
v. Mtumishi anayetarajia kustaafu kwa hiari au kwa lazima karibuni, anashauriwa kutoomba.

Mikopo hii ya Serikali haina riba bali mwombaji atakatwa **4%** ikiwa (**1% ni bima ya mkopo** na **3% ni ushuru wa huduma (Service Levy).**

**Viwango vya Mikopo**

i. Ngazi ya Mshahara (TGTS/TGHS/TGS/TGOS) A-C Tsh.15,000,000/= (Kiwango cha Juu)
ii. Ngaziya Mshahara (TGHS/TGTS/TGS) D-F Tsh.30,000,000/= (Kiwango cha Juu),
iii. Ngazi ya Mshahara (TGHS/TGTS/TGS) G-H Tsh.40,000,000/= (Kiwango cha Juu)
iv. Ngazi ya mshahara LSSE Tsh.50,000,000/=

**Uwasilishaji wa maombi;**

Watumishi wote wenye sifa zilizoainishwa hapo juu wawasilishe maombi yao kupitia Mfumo wa **Hazina "Portal"** kuanzia tarehe ya tangazo hili yaani **24.03.2025** hadi **30.03.2025**

# HATUA ZA KUJISAJILI KWENYE MFUMO WA HAZINA PORTAL

Zifuatazo ni hatua za kujisajili kwenye mfumo wa hazina

1. Fungua kivinjari unachopenda kutumia yaani "google chrome", "Mozilla fire Fox"
2. Andika kiunganishi cha **Als.muse.go.tz**
3. Utafunguka ukurasa wa **Hazina "Portal**"
4. Gusa mahali palipo andikwa "**REGISTER"**
5. Utafunguka ukurasa mpya wa kujaza taarifa za mtumishi husika mf check no, majina kamili ya mtumishi, tarehe ya kuzaliwa, vote code, sub vote code, salary acc namba (NMB, CRDB), salary scale, salary grade, salary step.
6. Bonyeza kitufe kilichoandikwa "**Verify details"** taarifa ulizozijaza zitaonekana na chini kabisa bofya "**Continue with Registration"**
7. Baada ya kuhakiki taarifa ukurasa mpya wa "**General Details"** utafunguka kukuruhusu kuendelea na usajili.
8. Hakikisha una taarifa zifuatazo
   - Active email (saw ana iliyopo kwenye mfumo wa HCMI
   - "Plot" namba
   - Namba ya nyumba
   - "Zip code" itumike 255
   - "Postal address"
   - "Confirmation date"
9. Baada ya kujaza taarifa zote sehemu ya "**General details**" utabonyeza "**Next"** Ukurasa mpya utafunguka "**Account Details"** sehemu hii utajaza User name (Check Number) na kutengeneza Nywila (Password) utakayoijaza sehemu ya "**Password"** na "**Confirm Password"** utabonyeza "**Register"**
10. Ujumbe wa kuthibitisha taarifa itatumwa kwenye **email** yako: ukisomeka noreply **Hazina "Portal User Email Verification"**
11. Ingia kwenye email thibitisha (verify acc) taarifa zako. Ukianza na **"Verify Email"** then "**Phone Verification"**

12. Ingiza Msimbo namba (OTP) zilizotumwa kwenye namba yako ya simu ilyokuwepo kwenye Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Mishahara (e-WATUMISHI) ili kuthibitisha
13. Baada ya kumaliza hatua za verification kwenye email
14. Ingia kwenye Mfumo (Log In) Kwa Kutumia Nywila Yako
15. Ukishaomba mkopo huu usi "with-draw" kwa kuwa utapoteza nafasi yako (que-position) maana mkopo huu unafuata kanuni ya FIFO-Firs In First Out yaani wa kwanza kuomba ndiye atakayekuwa wa kwanza kupata mkopo.

NB: "**Vote code**" na **"sub vote code"** zinapatikana kwenye hati za mishahara (salary slip)

- Hakikisha taarifa za awali kabla ya ku verify taarifa zako zinafana na zilizopo Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Mishahara **(e-WATUMISHI)**
- Endapo utakutana na changamoto katika usajili au wakati wa maombi ya mkopo kwenye Mfumo wasiliana na wafuatao;

1. Cecylia Lyoka-Mwakilishi wa Mikopo ya Hazina (Afisa Utumishi)-0629-387262/0748-986 118

2.Jackson Mwang'ombola (IT)-0620 347 962

**24.03.2025**

Grace A. Mhagama
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**TUNDURU**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
TUNDURU